

Je, Ni Vizuri Kufundisha Neno La Mungu Kwenye Msiba?

1. Kwanza ni jambo nzuri kwa kila mtu kusaidia majirani zao au ndugu wao katika vilio. Kwa sababu ni nafasi nzuri kuongea nao kuhsuu kifo na uaminifu wao. Ndio maana ni lazima kila mkusanyiko ya Bwana wawe tayari kutembea na kusaidia waliofiwa.
2. Katika Warumi 12:15 Paulo aliandika ni lazima, “Furahini pamoja nao wafurahio; lieni pamoja nao waliao.”
3. Kwa hiyo kufundisha mausia ya Mungu katika vilio ni vizuri sana na muda ni mzuri. Ni kwa sababu waliofia wanafikiri kifo na wanafikiri juu ya maisha badaa ya kufa. Kwa hiyo kuna watu wengi hapa ulimwenguni wamewahi kuokolewa kwa sababu mkristo alienda kwenye kilio na kufundisha ukweli wa Mungu.

Sasa Tufundishe Kwa Namna Gani Waliofiwa?

1. Kwanza ni lazima kila mwalimu aangalia mahitaji ya waliofiwa. Na bada ya kutambua mahitaji yao, kutuo huduma haraka sana kwa kila njia. Kama wanahitaji pesa, toa. Kama wanahitaji chakula, pika basi. Mara nyingi waliofiwa hawana uwezo wa kufanya chochote kwa sababu ya huzuni kubwa, lakini tukisaidia kwa pesa na chakula waliofiwa watakumbuka mpaka siku za mwisho.
2. Pia ni lazima kuwafariji waliofiwa kwa kuongea nao. Kwa kuongea maneno ya hekima na upendo. Tuonyeshe kweli tunajali. Daudi aliwai kulia kwa kuwa hakuona mtu yoyote aliyejali maisha yake. Tusiwape watu nafasi ya kuwa na mawazo kama haya leo. Tuwaonyeshe tunajali.

Kama Nitachagua Kutembea Katika Vilio, Ni Laizma Nifanye Nini Ili Nipate Matokeo Mazuri?

1. Kwa waliofiwa ni lazima tuonane nao haraka iwezekanavyo. Lakini pale pale ni vizuri tupande mbegu tu. Halafu baada ya siku tatu au nne, utaweza kufundisha waliofiwa vizuri. Mara nyingi kufundisha mkutano ya watu waliokusanyika ni rahisi muda wowote lakini waliofiwa ni vizuri kukaa nao bada ya siku chache, kwa kuwa siku ya kwanza wana huzuni tupu, hawatakaribisha masomo.
2. Pia uwe tayari kusaidia kitu cho chote. Ukiona kwa zile siku chache unawasaidia sana watafurahi kuongea na wewe baadae kuhusu maandiko. Lakini ukienda siku ya kwanza bila kutoa msaada inaweza kuwa vigumu kurudi badai.
3. Tena hata ukipata nafasi ya kuongeo nao siku ya tatu au nne, ni lazima urudi baada ya siku chache. Kwa kuonyesha huruma na upendo wako na kwa kupata nafasi ya kuendelea na kufundisha vizuri.

Kwa ufupi, kwenda kwenye vilio na kusaidia na kufundisha ni njia nzuri sana ya kujenga mwili wa Yesu Kristo. Sisi ni wanajeshi, ni lazima tuwe tayari kufundisha kila wakati tukipata muda.